

Sheria ya afya ya akili iwalinde walengwa

Na deogratias Mruah

Changamoto za maisha ya kisasa, utandawazi ikiwa ni pamoja na umasikini uliokithiri, ugonjwa wa UKIMWI, na matumizi ya madawa ya kulevya vinachangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa kasi ya idadi ya watu wanaosumbuliwa na maradhi ya akili hapa nchini. Pamoja na ongezeko kubwa la wagonjwa hawa bado jamii pamoja na serikali haijaoonyesha msukumo mkubwa katika kuhakikisha kuwa wenzetu hawa wanapata uangalizi na matibabu yanayofaa.

Kwa mujibu wa ripoti ya shirika la afya ulimwenguni juu ya hali ya afya kwa mwaka 2008, idadi kubwa ya watu wanaosumbuliwa na na maradhi ya akili katika nchi zinazoendelea hawapatiwi matibabu wala uangalizi wa kuwasaidia kudhibiti hali yao. , ripoti hiyo inaeleza katika Afrika inasemekana watu tisa kati ya kumi wanaougua maradhi ya kifafa hawapatiwi matibabu.

Hali hii inathibitika katika mipango ya afya ya halmashauri nyingi hapa nchini kushindwa kutoa kipaumbele katika huduma za afya ya akili. Matokeo yake ni idadi ndogo tu wagonjwa wa akili ambao hupatiwa huduma tena chini ya wahudumu wanaofanya kazi katika mazingira magumu.

Kuna uhaba mkubwa wa hospitali na vituo vya kutibu maradhi ya akili nchini na hata hivyo vichache vilivyopo havina watoa huduma wa kutosha. Kwa mfano hospitali ya rufaa ya magonjwa ya akili ya Mirembe ina daktari bingwa mmoja huku ikiwa na upungufu wa madaktari 150. Ni wazi kwa kuangalia hospitali hii kubwa hali itakuwa mbaya zaidi katika hospitali za mikoa na wilaya.

Sambamba na hilo pia jamii inagubikwa na unyanyapaa kwa wagonjwa wa akili huku mateso na manyanyaso kwa wenzetu hawa yakionekana kama kitu cha kawaida katika jamii. Kuna taarifa nyingi za kubakwa na kunyanyaswa kijinsia wanawake wenye matatizo ya akili huku jamii ikilifumbia macho suala hili.

Kulindwa na kupatiwa msaada unaofaa kutoka kwa mamlaka husika na jamii ni haki ya kikatiba wanayostahili watu wenye maradhi ya akili kama ilivyoainishwa katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 11(1). ***‘Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya mtu kufanya kazi kujipatia elimu na haki ya kupata msaada kutoka katika jamii wakati wa uzee, maradhi au hali ya ulemavu, na katika hali nyinginezo za mtu kuwa hajiwezi.....’***

Kwa kutambua haki hii ya watu wenye maradhi ya akili na kutoa msukumo wa jamii kushiriki katika kuwatunza watu wenye maradhi haya, bunge lilipitisha muswada wa sheria ya Afya ya Akili wa mwaka 2008 na kuidhinishwa kuwa sheria kamili baada kusainiwa na rais Disemba mwaka huohuo. Sheria hii inakusudia kuishirikisha jamii katika ufuatiliaji, utoaji wa huduma za afya na kulinda haki za watu wenye ugonjwa wa akili.

Ni vyema basi jamii kuwakumbuka watu wote wanaoteseka na maradhi ya utimamu wa akili kwa kuwatunza, kuwapatia haki wanazostahili na matibabu. Mipango ya afya kuanzia ngazi za familia hadi halmashauri lazima pia izingatie kundi hili na mahitaji yake. Ni jukumu la wizara inayohusika na usimamizi wa sheria ya afya ya akili ksimamia ipasavyo sheria hii ilikuweza kutimiza madhumuni ya kuanzishwa kwake. Ni vyema pia wizara ikahakikisha sheria hii inajulikana na watu wengi zaidi hasa vijijini ili kurahisisha matunzo ya wenzetu hawa wanaosumbuliwa na magonjwa ya akili. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuwatunza wagonjwa wa akili kwani nao wana haki ya kupata hifadhi hiyo katika jamii.